



# ARUSHA MEAT COMPANY LTD

P.O.BOX 14167  
ARUSHA  
TANZANIA  
TEL: +255272970304  
Mob: +255734026767  
E-mail: [arushameatcompany@yahoo.com](mailto:arushameatcompany@yahoo.com)

**KUMB. NA. AMCL/MTNZ/78/65**

**DATE: 07/11/2024.**

## TANGAZO LA NAFASI YA KAZI.

Arusha Meat Company Limited ni Kampuni iliyosajiliwa kwa mujibu wa sheria za Makampuni ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo inajishughulisha na huduma ya uchinjaji wa ng'ombe, mbuzi na kondoo. Aidha Kampuni hii pia huchakata nyama kwa ajili ya kutengeneza bidhaa mbalimbali. Arusha Meat Company Limited inakaribisha waombaji wenye sifa kujaza **nafasi mbili (02)** zilizowazi kama ifuatavyo:

### **1.0 AFISA UTUMISHI MSAIDIZI (ASSISTANT HUMAN RESOURCE OFFICER NAFASI MOJA (1)).**

#### **1.1 MAJUKUMU YAKE YATAKUWA KAMA IFUATAVYO;-**

- i) kushiriki katika kutunza kumbukumbu sahihi za watumishi wote wa Kampuni.
- ii) Kutafsiri na kushughulikia utekelezaji wa sheria na miongozi ya utumishi.
- iii) Kutafiti, kuchanganua na kukadiria idadi ya watumishi wanaohitaji mafunzo.
- iv) Kushiriki, na kuratibu zoezi la kupima utendaji kazi wa watumishi (Performance Apraisal) kwa kushirikiana na wakuu wa Idara.
- v) Kuandaa na kupanga mipango ya mafunzo ya muda mfupi na mrefu kwa watumishi.
- vi) Kukusanya, kuchambua na kupanga takwimu na kumbukumbu zote zinazohusu mipango ya watumishi.
- vii) Kuratibu likizo za watumishi wote wa Kampuni.
- viii) Atafanya jukumu jingine lolote linaloendana kulingana na majukumu atakayopangiwa na msimamizi wake wa kazi.

#### **1.2 SIFA ZA MWOMBAJI.**

Awe na stahhada ya Sayansi ya jamii au Sanaa kutoka katika vyuo vinavyotambuliwa na serikali na kujiimarisha (major) katika mojawapo ya fani zifuatazo:

- i) Menejimenti ya Rasilimali watu (Human Resource Management)
- ii) Elimu ya Jamii (Sociology).
- iii) Utawala na Uongozi (Public Administration)
- iv) Mipango ya Watumishi (Manpower Planning)
- v) Awe na ujuzi wa kutumia Kompyuta.

#### **MSHAHARA:**

Kwa kuzingatia ngazi za Mishahara ya Arusha Meat Company limited yaani ngazi ya **AMC 3**.

### **2.0 DEREVA (NAFASI 1)**

#### **2.1 MAJUKUMU YAKE YATAKUWA KAMA IFUATAVYO;-**

- i) Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari.
- ii) Kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi.
- iii) Kuwezesha usafirishaji wa mizigo/nyaraka za Kampuni, wageni na wafanyakazi wa ofisi pale itakapohitajika kufanya hivyo;
- iv) Kuhakikisha gari muda wote lipo katika hali ya usafi.
- v) Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari.
- vi) Kufanya jukumu jingine lolote atakalopangiwa na msimamizi wa kazi.

#### **2.2 SIFA ZA MWOMBAJI.**

- i) Mwombaji awe na cheti cha kidato cha nne (Form iv)
- ii) Awe na leseni ya udereva daraja D, E. Mwenye daraja C atapewa kipaumbele.
- iii) Awe na uzoefu wa kuendesha magari usiopungua mwaka mmoja (1) bila kusababisha ajali.
- iv) Awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji magari (Basic Driving Course) yanayotolewa na Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) au Chuo kingine kinachotambuliwa na Serikali na kutunukiwa cheti cha kuhitimu mafunzo hayo.
- v) Awe na umri usiozidi miaka 45.

#### **MSHAHARA:**

Kwa kuzingatia ngazi za Mishahara ya Arusha Meat Company limited yaani ngazi ya **AMC1**

### **MASHARTI YA JUMLA KWA NAFASI ZILİYOTANGAZWA.**

- i. Waombaji wawe raia wa Tanzania.
- ii. Waombaji waambatanishe Cheti cha kuzaliwa.
- iii. Waombaji waambatanishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed C.V) yenye anuani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (referees) watatu pamoja na barua iliyoandikwa kwa mkono na kusainiwa.
- iv. Anuani na namba ya simu ya mwombaji na picha moja "Passport size" ya hivi karibuni iandikwe jina kwa nyuma.
- v. Maombi yote yaambatane na nakala za vyeti vya taaluma, nakala za vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika vyeti vya kitaaluma (professional certificate) kutoka bodi husika na viwe "Certified".
- vi. "Testimonials", "provisional results", "statement of result" hati ya matokeo ya kidato cha nne na sita **HAVITAKUBALIWA.**
- vii. Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na mamlaka husika (TCU, NECTA, NACTE).
- viii. Mwombaji atajigharamia mwenyewe wakati wa usalli.
- ix. Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu ulioainishwa katika tangazo hili **HAYATAPOKELEWA.**
- x. Ajira hii ni ya mkataba wa muda maalum.
- xi. Barua zote zielekezwe kwa;  
MENEJA MKUU,  
ARUSHA MEAT CO. LTD,  
S.L.P 14167,  
**ARUSHA-TANZANIA.**
- xii. Barua zote za maombi zitumwe kwa njia ya Posta au kwa njia ya barua pepe (email) **recruitment@arushameat.co.tz.**
- xiii. Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 21/11/2024.

**NB: Barua zote zitakazotumwa nje ya utaratibu huu uliolekezwa katika tangazo hili hazitafanyiwa kazi.**

Tangazo hili limetolewa na: -

**MENEJA MKUU**  
ARUSHA MEAT CO. LTD